

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

Unapojibu tafadhalii taja:

Kumb. Na. CC/KMC/A.01/31/14

14 Februari, 2022

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni anapenda kuwatangazia Nafasi za Ajira ya Muda Nafasi **Mia Mbili Hamsini (250)** za Wakusanya Taarifa kwenye zoezi la Anwani za Makazi katika Kata na Mitaa yote ya Manispaa ya Kinondoni.

A. SIFA ZA WAOMBALI

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye Umri kati ya **Miaka 18-35**
- ii. Awe na elimu kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea.
- iii. Awe anamiliki simu janja Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na Barua pepe (email address) na Nywila (password) inayofanya kazi.
- v. Awe na uwezo wa kusoma Ramani za Mitaa.
- vi. Awe ni Mkazi wa Mtaa husika.

B. KAZI NA MAJUKUMU

- a) Kugawa/kuandika Namba za Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma
- b) Kukusanya taarifa za Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma
- c) Kukusanya taarifa za Wamiliki wa Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma kwa kutumia Mfumo wa Anwani za Makazi
- d) Kutuma Data kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi.

C. MALIPO

Kazi hii itafanyika kwa muda wa **Siku 45** kwa malipo ya **Shilingi 30,000/=** kwa siku

D. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;

1. Nakala ya cheti cha Kidato cha Nne na kuendelea
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Picha (passport size 2).

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na Anwani kamili ya mwombaji, namba ya Simu, Barua pepe na zipitie kwa Watendaji wa Mitaa na Kata anapoishi na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kwa anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA,
MANISPAA YA KINONDONI,
S.L.P 31902,
DAR ES SALAAM**

F. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **16/02/2022** Saa **9.30** Alasiri.


Hanifa S. Hamza
MKURUGENZI WA MANISPAA

*MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI
DAR-ES-SALAAM*